JAMHULI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR-TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MTWARA

0713-830862 / 0682870875

SHULE YA SEKONDARI MUSTAFA SABODO, S.L. 158 MTWARA

MAELEKEZO UA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

MZAZI/MLEZI WA: ……

Ninayo furaha kukujulisha kwamba mtoto wako ……

Ni miongoni mwa Wanafunzi walioteuliwa kujiunga na Shule ya Sekondari **MUSTAFA SABODO** kidato cha kwanza **2021.** Shule ipo Mkoa wa **Mtwara,** Wilaya ya **Mtwara,** umbali wa **km 17** kutoka Mtwara mjini kwenye barabara iendayo **Masasi** na **Lindi**. Usafiri wa basi/daladala unapatikana kwa urahisi kutoka stendi kuu Mtwara nauli ya shilingi elfu moja tu.

Anatakiwa kufika hapa shuleni tarehe **10/01/2021** bila kukosa. Aidha mwanao atajiunga na shule hii baada ya kutekeleza masharti yafuatayo:-

(a) AFYA

Awasilishe hapa shuleni fomu “request for medical Examination” iliyojazwa na daktari yeyote wa hospitali ya serikali baada ya kupimwa. Fomu hiyo imeambatanishwa na barua hii.

(b) KAZI ZA MIKONO

Aje na ndoo 2 ndogo, jembe lenye mpini, fagio ya chelewa, fyekeo na panga kwa ajili ya kazi za mikono.

(c) SARE YA SHULESARE YA SHULE

(d)

(e) C 1. WASICHANA

(i) Awe na Sketi mbili rangi ya bluu bahari rinda box **(UREFU WAKE UKARIBIE FUNDO LA MIGUU)** na shati mbili nyeupe mikono mifupi. Au **NUSU KANZU** mbili nyeupe **ZISIZOBANA**, mikono mirefu na juba mbili rangi nyeupe za KUSHONWA (**ZINAZOFIKA USAWA WA KIUNO**) na kofia nyeupe ya kichwani.

(ii) Awe na jozi mbili za viatu vya ngozi vyeusi vya kamba, viwe visigino vifupi

(iii) Awe na jozi mbili(2) za soksi nyeupe, ziwe ndefu (stokingi)

(iv) Sketi mbili nyeusi na fulana 2 za bluu kwa ajili ya kushindia na kazi za nje au nusu kanzu mbili za blue zisizobana, mikono mirefu na juba mbili rangi ya blue za kushonwa na kofia ya blue ya kichwani. **(urefu wa sketi ukaribie kwenye fundo la miguu)**

(v) Awe na nguo za ndani za kutosha pamoja na taulo za kike (pedi) za kutosheleza muhula mzima

C2. WAVULANA

(i) Awe na suruali mbili rangi ya bluu bahari zilizoshonwa kiheshima (zisishonwe katika mtindo wa jeans na zisibane)
(ii) Awe na mashati mawili meupe ya mikono mifupi isiyobana
(iii) Awe na jozi mbili (2) za soksi nyeupe
(iv) Awe na jozi mbili (2) za viatu vyeusi vya kamba, viwe na visigino vifupi
(v) Suruali 2 nyeusi na fulana 2 za bluu kwa ajili ya kushindia na kazi za nje
(vi) Awe na mkanda mweusi wa ngozi.

MUHIMU SANA: Suruali ziwe na upana ambao ikivutwa juu ivuke magoti kwa urahisi. **(zisiwe "Chupa")**

(f) VIFAA VISAIDIZI KWA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUMU

- ✓ **d1.** Mwanafunzi mwenye ulemavu wa ngozi (Albino)
  Aje na vifaa vifuatavyo:- Mafuta na kofia za kujikinga na jua au mwanga mkali
- ✓ d2. Mwanafunzi mwenye usikivu hafifu.
  Aje na vifaa saidizi vya kuongeza usikivu (hearing aids) na kamusi ya CHAVITA ya lugha ya alama.
- ✓ d3. Mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo ambaye hajimudu kutembea mwenyewe
  aje na vifaa wezeshi kama vile:- baiskeli, viatu, fimbo na magongo kulingana na tatizo lake.
- ✓ d4. Mwanafunzi mwenye uoni hafifu
  Aje na vifaa vya kukuza maandishi (magnifiers)

- ✓ **KWA WANAFUNZI WAGONJWA WAJE NA VYETI VYA KUONYESHA UGONNJWA NA BARUA YA MZAZI YA KUONYESHA JUHUDI YA MATIBABU ALIYOYAFANYA NA KAMA MTOTO HANA UGONJWA UNAOMSUMBUA MTOTO MARA KWA MARA MZAZI AELEZE KUWA MTOTO HANA TATIZO KUBWA LINALOMSUMBUA MTOTO**.
  MWANAFUNZI MGONJWA ATAKAEFIKIA HATUA YA KUSHINDWA HATA KUTEMBEA ,**MZAZI ATAMFUATA NA KWENDA NAE NYUMBANI MPAKA ATAKAPOPONA.**

<u>MENGINEYO</u>

(i) Godoro futi $2^1/_2$ x 6 , shuka mbili za kitanda rangi ya bluu.
(ii) Awe na Daftari kubwa (counter) za masomo anayosoma
(iii) Awe na seti ya hisabati (mathematical set) na ruler moja.
(iv) Awe na vifaa vya michezo (Jezi) fulana na bukta za blue na viatu/ raba za michezo jozi moja (1).
(v) Awe na nguo za michezo trakisuti (chini na juu) rangi ya bluu iliyoiva.
(vi) Kadi ya mfuko wa matibabu/ gharama ya matibabu litakuwa jukumu la mzazi/ endapo mwanafunzi hana bima ya afya aje na Sh 5,000/ kwa ajili ya kutengenezewa bima ya mwaka mmoja ya **CHF**
(vii) Vifaa kwa ajili ya kuwekea chakula (kontena lenye funiko), kikombe na kijiko.
(viii) Neti ya mbu. (ix) **Potifolio (file la kutunzia kumbukumbu za mitihani**)
(x) Sanduku la chuma. (xi) Kamusi ya kiingereza. (xii) Nakala ya hati/cheti cha kuzaliwa

(g) VIFAA VISAIDIZI KWA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUMU

d1. Mwanafunzi mwenye ulemavu wa ngozi (Albino)
Aje na vifaa vifuatavyo:- Mafuta na kofia za kujikinga na jua au mwanga mkali

d2. Mwanafunzi mwenye usikivu hafifu.
Aje na vifaa saidizi vya kuongeza usikivu (hearing aids) na kamusi ya CHAVITA ya lugha ya alama.

d3. Mwanafunzi mwenye ulemavu wa viungo ambaye hajimudu kutembea mwenyewe
aje na vifaa wezeshi kama vile:- baiskeli, viatu, fimbo na magongo kulingana na tatizo lake.

d4. Mwanafunzi mwenye uoni hafifu
Aje na vifaa vya kukuza maandishi (magnifiers)

SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE KWA KILA MWANAFUNZI

1. Atii sheria, kanuni na taratibu zote zilizowekwa na shule
2. Afanye kazi za mikono nje ya darasa na ajifunze masomo darasani kwa juhudi na maarifa
3. Awatii na awaheshimu wazazi/walezi wake, waalimu, wafanyakazi wasio waalimu na watu wengine wote wasiomzidi umri.
4. Atasimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri apitapo, aingiapo mahali popote atakapokuwa.
5. Awe katika sare ya shule wakati wote awapo shuleni
6. Ahudhurie vipindi vyote bila kukosa, na awepo shuleni au darasani kwa siku zote za masomo.
   - Mwenye suala la msingi la kumfanya atoke nje ya shule wakati wa masomo, atapewa kibali cha maandishi na mwalimu mwenye dhamana ya kutoa ruhusa
   - Mgonjwa ataomba ruhusa kwa mwalimu wa darasa lake na kuruhusiwa na mwalimu wa zamu. Arudipo shuleni atawasirisha vyeti vya matibabu kutoka kwa daktari
7. Awepo mahali anapotakiwa kuwa kwa wakati.
8. Asiyewahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba atachukuliwa hatua za utovu wa nidhamu.
9. Haruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu wake na kwa watu wengine.
10. Awe mfano mzuri wa heshima na tabia njema na mahali popote awapo.
11. Aheshimu na kukubalui tofauti za kisiasa, kidini na kitamaduni zilizopo katika jamii.
12. Avalie suruali/ sketi kiunoni, Hairuhusiwi kuvaa debweza au namna nyingine yeyote.
13. Atakwenda sehemu zifuatazo kwa kutumwa na mwalimu au mfanyakazi asiye mwalimu. Chumba cha walimu, ofisi za shule, maabara, jikoni, nyumba za wafanyakazi (wasio walimu au walimu)
14. Awe nadhifu wakati wote.

    Yafuatayo ni baadhi ya mambo yanayoweza kusaidia kumfanya mwanafunzi kuwa nadhifu

    Kukata kucha, kunyoa ndevu (wavulana) kuvaa nguo safi na za heshima, kukata nywele na kuwa fupi, kutojirembesha na kutopaka madawa kwenye ngozi na nywele, kupiga viatu kiwi, kufunga mkanda.
15. Awe mzalendo

    Viashiria vya uzalendo ni kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
16. Mwanafunzi anaweza kufukuzwa shule kwa kutenda makosa yafuatayo:-
    i. Wizi
    ii. Uasherati na ushoga
    iii. Ubakaji

iv. Ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
v. Makosa ya jinai
vi. Kupigana, kupiga
vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
viii. Kudharau bendera ya taifa
ix. Kuoa au kuolewa
x. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
xi. Kutoa mimba
xii. Kuvuruga amani na usalama wa watu.
xiii. Kukataa adhabu kwa makusudi
xiv. Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo
xv. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

17. Awe mwangalifu ili aweze kuepuka maovu.
18. Wazazi, walezi, ndugu na jamaa wataruhusiwa kuwaona wanafunzi jumapili ya mwisho wa mwezi tu.

ANGALIA KWA MAKINI:

(i) Kila mzazi/ mlezi wa mwanafunzi azisome sheria / kanuni na taratibu kwa uangalifu.
(ii) Karatasi zilizoambatanishwa zishughulikiwe ipasavyo na zirejeshwe suleni zikiwa zimejazwa kwa ukamilifu.

RIYADH KADHI

MKUU WA SHULE

UTHIBITISHO WA MZAZI

KUHUSU TABIA NA MWENENDO WA MWANAFUNZI

Mimi ……ninakubali mwanangu……..…..asome katika shule ya sekondari ya bweni ya MUSTAFA SABODO kuanzia mwezi wa ……mwaka 20……..

Nimezisoma na kuzielewa SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE KWA MWANAFUNZI.

ninaahidi kuwa nitajitahidi kadiri ya uwezo wangu kuhakikisha kwamba anatii sheria, kanuni na taratibu zote za shule wakati wote atakapokuwa anasoma hapa shuleni.

pale atakaposhindwa kuzitii sheria hizo hatua yeyote ya kinidhamu ichukuliwe dhidi yake.

Anuani ya Kijiji/Mtaa:…….

Kata:…….

Wilaya:…….

Mkoa:……

Nambari yangu ya simu ……

Sahihi ya mzazi/ mlezi ……

Tarehe ……

SAHIHI YA MWANAFUNZI …….

Tarehe ……

Jina na sahihi ya mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa

1…… Sahihi……..

2…… Sahihi …….

Mhuri wa Serikali ya Kijiji/Mtaa:

……

THE HEAD MASTER
MUSTAFA SABODO SEC SCHOOL
P.O.BOX 158
MTWARA
Date …….

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM.
To be completed by a medical officer in respect of all form one entrant.
Full name ……
Age ……
Blood count (red and white)
……..
Stool examination
……
Urine analysis
……
Syphilis test
……
Eye test ……
Ears ……
Chest ……
Pregnancy ……
Abdomen ……
Additional information e.g. physical defects or impairment(s)
……
……
Infection, or chronic or family diseases
……..
……

I certify that I examined the above named boy/girl and I find him/her physically and mentally fit/unfit to pursue the courses as stated above.
Signature ……
Designation ……..
Station ……
Date ……

N:B: Medical officer, at the time of examination, please treat the individual for any ailment you note.

SHULE YA SEKONDARI MUSTAFA SABODO SLP 158. MTWARA

TAARIFA MUHIMU KUHUSU MWANAFUNZI MPYA.

SEHEMU A.

JINA KAMILI .....

TAREHE YA KUZALIWA

.....

KABILA .....

JINA LA BABA .....

JINA LA MAMA .....

ANUANI YA NYUMBANI/ KIJIJI

.....

SEHEMU B

KAZI YA BABA/ MLEZI

.....

KAZI YA MAMA/MLEZI

.....

BABA ANAISHI/AMEFARIKI

.....

MAMA ANISHI/AMEFARIKI

.....

NAMBA YA SIMU YA BABA/MAMA/ MLEZI

.....

SEHEMU C

MAJINA YA NDUGU KUFUATA UMRI WAO

NA	JINA LA NDUGU	JINSIA	UMRI	KIWANGO CHA ELIMU
1				
2				
3				
4				
5				

SEHEMU D

UONGOZI NA MADARAKA ULIYOWAHI KUSHIKA

AINA YA MADARAKA	SHULE/MAHALI	TOKA MWAKA	HADI

SEHEMU E.

MAMBO UNAYOPENDELEA MBALI NA MASOMO YA DARASANI, MFANO; MICHEZO, NGOMA, UTUNZAJI WA MAZINGIRA N.K

1. .....
2. .....